

## **ROZARI YA UTATU MTAKATIFU.**

*Inaaminika kwamba imefunuliwa na Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste 26 Mei, 1996(unaweza kutumia Rozari ya kawaida)*

### **NAMNA YA KUSALI**

- (1) Kwenye Msalaba: **Kanuni ya Imani inayotumika kwenye Rozari**
- (2) Kwenye chembe kubwa baada ya Msalaba: **Baba Yetu**
- (3) Kwenye chembe tatu ndogo: **Salamu Maria**
- (4) Kwenye chembe kubwa baada ya kila fungu: **Atukuzwe Baba**
- (5) Kwenye chembe ndogo, kumi kumi kila fungu:

**K.** Ee Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, nakuabudu, nakufariji, nakupenda,

**W.** Kwa njia ya Maria, kwa Maria, Pamoja na Maria na ndani ya Maria Bikira daima, Mtakatifu na Mkingiwa dhambi ya asili, Binti wa Mungu, Mama wa Mungu na Bi-arusi wa Mungu. Amina

### **LITANIA YA UTATU MTAKATIFU**

Mungu Baba wa mbinguni,.....utuhurumie

Mungu mwana mkombozi wa dunia,.....utuhurumie

Mungu Roho Mtakatifu,.....utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu sana, Mungu Mmoja,...utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu sana, umoja usiogawanyika,

Mkuu sana kuliko wote walio na utakatifu,.....utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu sana, Mungu wa Kweli na

Mungu mmoja.....utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu sana, utukufu wa enzi yako,,.....utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu, Mwenyezi na utatu wa Mungu

Wa milele.....Utuhurumie

Ee utatu Mtakatifu sana, ambaye anaishi ndani mwangu...utuhurumie

Ee Utatu Mtakatifu sana, wenye nguvu kuliko wote,.....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, wenye mastahili sana ya sifa zote...utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, Mfalme na tegemeo la mioyo yote,....utuhurumie  
Ee utatu Mtakatifu sana, unayetajirisha wote wanaokuomba,....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, chemichemi ya uhai na utakatifu.....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, chanzo cha vitulizo vyote.....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, Matumaini ya wote wanaokufa katika wewe,....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, uzuri wa watakatifu wote,.....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, wenye utakatifu sana na ukuu wa juu sana,.....utuhurumie  
Ee Utatu Mtakatifu sana, ufalme ni wako na nguvu.....utuhurumie.  
Ubarikiwe Roho Mtakatifu Mfariji,.....ubarikiwe Mungu katika enzi yako  
Ubarikiwe Mungu Mwenyezi na wa milele, .....ubarikiwe Mungu katika enzi yako  
Libarikiwe Jina lake Takatifu.....ubarikiwe Mungu katika enzi yako  
Ubarikiwe Mwenye utukufu mkuu Zaidi kuliko majina yote...ubarikiwe Mungu katika enzi yako  
Ubarikiwe Utukufu wenye enzi, Bwana Mkuu, mmoja katika utatu.....ubarikiwe Mungu katika enzi yako  
Ubarikiwe Mungu katika Malaika na Watakatifu wako.....ubarikiwe Mungu katika enzi yako.

### **Sala ya Waabuduo**

*(imefundishwa na Malaika wa Mungu kwa Watoto watatu wa Fatima mwaka 1997)*

Ee Mungu wangu, nakuamini, nakuabudu, nakutumaini, nakupenda! Naomba toba na msamaha kwa ajili ya wale ambao hawakuamini, wala hawakuabudu, wala hawakutumaini na wala hawakupendi. Ee Utatu Mtakatifu sana, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, nakuabudu ndani kabisa ya mtima wangu! Nakutolea Mwili Azizi sana, Damu, Roho na Umungu wa Bwana wetu Yesu Kristu, uliyepo katika Tabernakulo zote duniani, kwa ajili ya fedheha kubwa, kufuru na ubaridi unaofanywa dhidi yako ambapo yeye mwenyewe anapata uchungu sana. Amina

### **Ahadi kwa wote watakaosali Rozari hii**

1. Watakaosali sala hii mara moja, hawataonja moto wa jahanamu. Amina
2. Watakaosali sala hii mara tisa(9) kwa siku katika Maisha yao ya hapa duniani, watapewa neema ya kuepuka moto wa toharani. Amina
3. Sala hii ikisaliwa mara moja roho za watu milioni moja hapa duniani, wana uhakika wa ukombozi Pamoja na neema za uzima wa milele mwisho wa Maisha yao ya hapa duniani, na pia roho za watu milioni mbili hutolewa toharani kwenda mbinguni. Amina
4. Utatu Mtakatifu sana na Bikira Maria, Mtumishi mnyenyekevu wa Bwana, wamehaidi kwamba, ombi lolote au upendeleo wowote utakaombwa utatolewa, hata kama kwa mtazamo wa kibinadamu haiwezekani, kutafanyika muujiza ikiwa ni lazima ili kutimiza kile kilichombwa kwa sahrti kwamba anayesali atafanya hivyo mara tisa kwa siku au atasali novena (siku tisa). Amina
5. Ikiwa sala hii ina nguvu ya kuokoa roho ya mtu anayekufa. Ikisaliwa mara moja kwa siku, mtu anayekufa ataokolewa na moto wa milele. Ikisaliwa mara tatu(3) anayekufa ataenda moja kwa moja mbinguni. Amina
6. Ikiwa salah ii itasaliwa mara moja kwa siku, watu tisa waliopagawa na mashetani na pepo wabaya mara moja watafunguliwa vifungo vyao na hawatapagawa tena. Na watu hawa watapata neema ya uzima wa milele. Amina
7. Wale ambao ni Watoto halisi wa Maria, wakisali sala hii mara tatu tu watapewa ulinzi wa mbinguni na neema ya kumwona Mwana wa Mungu Yesu Kristu akija duniani mara ya pili. Amina